

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**TAASISI YA ELIMU TANZANIA**



**MTAALA WA MAFUNZO YA ASTASHAHADA  
YA UALIMU ELIMU MAALUMU TANZANIA**

© Taasisi ya Elimu Tanzania, 2019

Toleo la kwanza 2019

ISBN: 978-9976-61-832-7

Taasisi ya Elimu Tanzania

S.L.P 35094

Dar es Salaam

Simu: +255222773005

Faksi: +2552227744420

Baruapepe: [director.general@tie.go.tz](mailto:director.general@tie.go.tz)

Tovuti: [www.tie.go.tz](http://www.tie.go.tz)

Mtaala huu urejelewe kama: Taasisi ya Elimu Tanzania. (2019). Mtaala wa Mafunzo ya  
Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu. Dar es Salaam:  
Taasisi ya Elimu Tanzania.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha wala kufasiri  
andiko hili kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu  
Tanzania.

## **Idhini**

Mtaala ni nyenzo muhimu ya ufundishaji na ujifunzaji katika ngazi yoyote ya elimu na huakisi ubora wa elimu inayotolewa. Lengo la mtaala huu wa Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu ni kumsaidia mkufunzi na wadau wa elimu maalumu nchini Tanzania kutoa elimu na malezi yenye viwango vya ubora vinavyokubalika kitaifa na kimataifa. Mtaala huu umeandaliwa ili kujenga umahiri kwa mwalimu tarajali utakaomwezesha kumudu ufundishaji na ujifunzaji katika shule za msingi. Mkufunzi hana budi kuupitia mtaala kwa umakini ili aweze kuwa na mtazamo mpana kuhusu kile anachotakiwa kukifundisha.

Ni matarajio yangu kuwa watekelezaji wa mtaala huu watamwezesha mwalimu tarajali kujenga umahiri uliokusudiwa kama ulivyoelekezwa katika mtaala huu.



Kaimu Kamishna wa Elimu  
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia  
S.L.P. 10  
Dodoma  
Simu: +255 26 296 3533  
Barua pepe: [info@moe.go.tz](mailto:info@moe.go.tz)  
Tovuti: [www.moe.go.tz](http://www.moe.go.tz)

## **Dibaji**

Mtaala wa Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu umeandaliwa ili kukidhi mahitaji ya upatikanaji wa walimu wa kufundisha wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika ngazi ya shule za msingi. Mtaala huu utawawezesha wakufunzi na wadau wengine wa elimu kufanikisha mafunzo ya ualimu ngazi ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu.

Mtaala huu una vipengele vikuu tisa ambavyo ni: utangulizi, muktadha wa sasa wa mtaala wa mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu unaozingatia mahitaji ya kijamii na kiuchumi, dira, dhamira, malengo na ujuzi wa jumla wa Mtaala, muda wa mafunzo, muundo wa maudhui, maeneo ya kujifunza na viwango vya rasilimali katika utekelezaji wa Mtaala. Vipengele vingine ni: njia za kufundishia na kujifunzia, upimaji wa maendeleo ya mwalimu tarajali, ufuatiliaji na tathmini ya Mtaala.

Mtaala unaelezea mazingira halisi ya sasa ya kijamii na kiuchumi ambapo utatekeleza na kubainisha malengo makuu ya elimu, Elimu ya Ualimu na Elimu ya Ualimu Elimu Maalumu. Pia, Mtaala umebainisha wazi umahiri ambao mwalimu tarajali anatakiwa kuujenga. Aidha, katika masomo, maeneo ya kujifunza na mgawanyo wake umeoneshwa wazi katika masomo ya fani, ualimu na yale ya ufundishaji ili kutoa mwongozo katika ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Vilevile, Mtaala unaeleza sifa anazopaswa kuwa nazo mkufunzi na kiongozi wa chuo pamoja na mahitaji ya rasilimali watu na vitu vinavyotakiwa chuoni. Muundo wa upimaji wa walimu tarajali katika mafunzo kwa vitendo umeoneshwa kwa ajili ya kuwawezesha kupata umahiri wa ufundishaji na ujifunzaji.

Mwisho, Mtaala unaeleza njia za ufuatiliaji na tathmini ya Mtaala ambazo zinatakiwa kutumika wakati Mtaala unatekelezwa na baada ya utekelezaji wake. Kwa ujumla, Mtaala umelenga kuwa mwongozo kwa wadau wote wa Elimu katika kuwezesha utekelezaji wenye ufanisi.



Dkt. Aneth A. Komba

Mkurugenzi Mkuu

Taasisi ya Elimu Tanzania

# YALIYOMO

Idhini .....	iii
Dibaji .....	iv
Orodha ya Majedwali.....	vii
Vifupisho .....	viii
1.0 Utangulizi .....	1
1.1 Sababu za Kuandaa Mtaala .....	1
1.2 Muundo wa Mtaala wa Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu .....	1
2.0 Muktaba wa Sasa wa Mtaala wa Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu .....	2
2.1 Mahitaji ya Kijamii .....	3
2.2 Mahitaji ya Kiuchumi .....	3
2.3 Matamko ya Sera .....	3
3.0 Dira, Dhamira, Malengo na Ujuzi wa Jumla wa Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu .....	7
3.1 Dira .....	7
3.2 Dhamira .....	7
3.3 Malengo ya Jumla ya Elimu, Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu na Ualimu Elimu Maalumu .....	7
4.0 Muda wa Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu .....	10
4.1 Miaka ya Mafunzo .....	10
4.2 Muda wa Masoma .....	10
4.3 Mihula ya Masomo .....	11
5.0 Muundo wa Maudhui, Maeneo na Masomo ya Kujifunza .....	11
5.1 Masomo ya Fani za Ualimu Elimu Maalumu .....	12
5.2 Masomo ya Ufundishaji .....	13
6.0 Viwango vya Rasilimali Katika Utekelezaji wa Mtaala .....	38
6.1 Sifa ya Kujiunga na Mafunzo .....	38
6.2 Sifa za Mkufunzi.....	38
6.3 Sifa za Kiongozi wa Chuo.....	38
6.4 Rasilimali vitu.....	39
7.0 Njia za Kufundishia na Kujifunzia .....	41

8.0	Upimaji wa Maendeleo ya Mwalimu Tarajali .....	42
8.1	Upimaji Endelevu .....	42
8.2	Utahini wa Mafunzo kwa Vitendo .....	42
8.3	Upimaji Tamati .....	43
8.4	Mtihani wa Mwisho .....	55
9.0	Ufuatiliaji na Tathmini ya Mtaala .....	56
9.1	Ufuatiliaji wa Mtaala .....	56
9.2	Tathmini ya Mtaala .....	57
Rejea	.....	59

## Orodha ya Majedwali

Jedwali la 1: Mchanganuo wa Vipindi kwa Wiki kwa Fani na Mchepuo.....	12
Jedwali la 2: Masomo katika Fani ya Ualimu Elimu Maalumu .....	12
Jedwali la 3: Michepuo na Masomo ya Ufundishaji katika Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu .....	14
Jedwali la 4: Umahiri Mkuu wa Masomo ya Fani kwa Mwalimu Tarajali ...	15
Jedwali la 5: Umahiri wa Jumla wa Somo na Umahiri Mkuu wa kila Fani kwa Masomo ya Ufundishaji kwa Mwalimu Tarajali .....	19
Jedwali la 6: Umahiri Mkuu wa Somo la Ualimu na Somo la Elimu Jumuishi.....	35
Jedwali la 7: Mpangilio wa Muda wa Mafunzo kwa Saa .....	37
Jedwali la 8: Upimaji wa Masomo ya Fani ya Astashahada ya Ualimu wa Elimu Maalumu .....	44
Jedwali la 9: Upimaji wa Masomo ya Mbinu za Kufundishia Masomo ya Elimu ya Msingi .....	53
Jedwali la 10: Ufuatiliaji wa Mtaala.....	57
Jedwali la 11: Tathmini Endelevu .....	58

## **Vifupisho**

KKK	Kusoma, Kuandika na Kuhesabu
MKUKUTA	Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania
TEHAMA	Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
TET	Taasisi ya Elimu Tanzania
UKIMWI	Upungufu wa Kinga Mwilini
VVU	Virusi vya UKIMWI
WyEST	Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia



## **1.0 Utangulizi**

Mtaala ni mwongozo mpana unaoweka viwango vya utoaji wa elimu kwa kuzingatia maudhui na ujuzi watakaojifunza walimu tarajali kama vile maarifa, stadi na mwelekeo, njia za kufundishia na kujifunzia zitakazotumika katika utekelezaji wa Mtaala, vifaa vya kufundishia na kujifunzia vinavyohitajika, sifa za kitaaluma na kitaalamu za mkufunzi atakayeuwezesha mtaala, miundombinu wezeshi katika utekelezaji wa Mtaala, muda utakaotumika katika ufundishaji na ujifunzaji, upimaji, ufuatiliaji na tathmini ya Mtaala. Kwa hiyo, Mtaala wa Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu una mtazamo wa kisasa unaoonekana kama ni kioo kinachoakisi falsafa na utamaduni wa jamii, vikiwamo vyanzo vya maarifa na malengo ya elimu ya nchi. Kioo hiki huonesha pia maarifa, stadi na mwelekeo unaotarajiwa kumjenga mlengwa kumudu kufundisha masomo ya elimu ya msingi kwa kuonesha njia za utahini, ufuatiliaji na tathmini.

### **1.1 Sababu za Kuandaa Mtaala**

Mtaala huu wa Astashaada ya Ualimu Elimu Maalumu umeandaliwa kwa kuzingatia Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025, Malengo ya Maendeleo Endelevu 2015-2030, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA), Mkakati wa Taifa wa Elimu Jumuishi wa mwaka 2009-2017 na Mkakati wa Taifa wa Elimu Jumuishi wa mwaka 2018-2021. Vilevile, Mtaala huu umezingatia mapendekezo ya tafiti anuwai za kielimu, hususani “Ripoti ya utafiti wa kuboresha Elimu ya Msingi Tanzania Bara” ya Agosti, 2004 na “Ripoti ya utafiti na maoni ya kuboresha Mtaala wa Mafunzo ya Ualimu Tarajali ngazi ya Astashahada” ya mwaka 2018. Matokeo ya utafiti na maoni ya wadau yalidhihirisha umuhimu wa kuboresha Mtaala uliokuwa ukitumika kuandaa walimu kwa njia ya mafunzo kazini katika fani za Ualimu Elimu Maalumu wa mwaka 2012 ili kuandaa Mtaala wa Ualimu Elimu Maalumu ngazi ya Astashahada.

### **1.2 Muundo wa Mtaala wa Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu**

Mtaala huu una sehemu tisa. Sehemu ya kwanza inahusu utangulizi wa mtaala.

Sehemu nane zinazofuatia katika Mtaala huu zinaelezea muktadha wa Mtaala wa Mafunzo ya Ualimu Elimu Maalumu unaozingatia mahitaji ya kijamii na kiuchumi, dira, dhamira, malengo na ujuzi wa jumla wa Mtaala, muda wa mafunzo, muundo wa maudhui, maeneo na masomo ya kujifunza, viwango vya rasilimali katika utekelezaji wa Mtaala, njia za kufundishia na kujifunzia, upimaji wa maendeleo ya mwalimu tarajali na ufuatiliaji na tathmini ya Mtaala.

Mtaala wa Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu utatekelezwa kwa ufanisi kwa kufuata mwongozo unaobainisha masuala muhimu ya elimu, ikiwa ni pamoja na matamko ya Sera ya Elimu (2014) inayoeleza malengo ya elimu Tanzania. Ieleweke wazi kuwa kuna malengo makuu ya kitaifa yanayotazamiwa kufikiwa pamoja na ujuzi wa jumla unaokusudiwa kujengwa kwa mwalimu tarajali katika Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu. Katika Mtaala huu, mambo yafuatayo yameainishwa: Muda wa mafunzo, maudhui, masomo na maeneo ya kujifunza, viwango vya rasilimali vinavyohitajika katika utekelezaji wa Mtaala, njia za kufundishia na kujifunzia, taratibu za upimaji wa mwalimu tarajali na ufuatiliaji na tathmini ya Mtaala.

## **2.0 Muktadha wa Mtaala wa Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu**

Madhumuni ya Elimu ya Ualimu Elimu Maalumu ni kujenga misingi ya kielimu, kijamii na kiutamaduni kwa mwalimu tarajali katika kuwezesha ujifunzaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Elimu hii inakusudiwa kumwezesha kila mwalimu tarajali kupata maarifa, mwelekeo, ujuzi na stadi za msingi za ufundishaji na ujifunzaji, ujasiriamali pamoja na misingi ya uongozi ili kukabiliana na changamoto mbalimbali katika mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Maendeleo makubwa na ya haraka katika sayansi na teknolojia na hasa teknolojia ya kupashana habari, yamesababisha mabadiliko makubwa ya uendeshaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii katika kila nchi ikiwa ni pamoja na utoaji wa elimu kwa watu wenye mahitaji maalumu. Hivyo, Mtaala wa Mafunzo ya Astashahada ya Elimu ya Ualimu Elimu Maalumu umezingatia mahitaji hayo.

## **2.1 Mahitaji ya Kijamii**

Tanzania ina jamii za watu wanaotoka katika makabila mbalimbali ambao wameunda Taifa moja linalotumia Kiswahili kama lugha ya mawasiliano. Lugha hiyo inawaunganisha watu hao katika shughuli zao za kila siku za maendeleo. Mtaala wa Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu umezingatia mahitaji ya kijamii kwa kutumia lugha ya Kiswahili inayoeleweka na inayotumiwa na watu walio wengi. Aidha, Mtaala umehusisha masuala mtambuka yanayohusu utandawazi, teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA), elimu ya jinsia na utawala bora. Pia, yanayohusu stadi za maisha, ujasiriamali, elimu jumuishi, maadili, ushauri na unasihi pamoja na huduma za faraja kwa wanaoishi na virusi vya UKIMWI.

## **2.2 Mahitaji ya Kiuchumi**

Tanzania ni nchi ambayo ina raslimali nyingi kama gesi asili, madini ya aina mbalimbali na mbuga za wanyama ambazo zinavutia watalii wanaotuletea fedha za kigeni. Hata hivyo, kutokana na maendeleo duni ya sayansi na teknolojia pamoja na kutokuwepo kwa usawa katika soko la dunia kumesababisha pato la nchi kuwa dogo na kufanya vyo vya elimu ya ualimu kutovutia wanafunzi wengi wa ualimu kujiunga navyo. Jitihada za makusudi zinahitajika ili kufanya kada ya ualimu kuwa kivutio kwa Watanzania. Kwa mantiki hiyo, Mtaala wa Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu umehusisha masuala ya ujasiriamali, stadi za kazi, michezo pamoja na sayansi na teknolojia ili kumwezesha mwalimu tarajali kujitegemea kwa kutumia elimu atakayoipata kutambua jinsi ya kutumia rasilimali zilizopo kupata mahitaji yake ya msingi na kumfanya kuwa na maendeleo endelevu yenye ufanisi katika jamii. Aidha, elimu itakayotolewa itaunganisha nadharia na vitendo ili kuleta tija kwa mwalimu tarajali na mwanafunzi atakayefundishwa na mwalimu huyo baada ya kuhitimu.

## **2.3 Matamko ya Sera**

Katika uboreshaji wa Mtaala huu wa Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu, sera mbalimbali za kimataifa na za kitaifa zimezingatiwa ili kumuandaa kikamilifu mwalimu tarajali aweze kupata elimu bora itakayomwezesha kuwa mwalimu mahiri wa Elimu Maalumu.

### 2.3.1 Sera za Kimataifa

Sera za kimataifa zilizingatiwa ni kama zifuatazo: Azimio la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu la mwaka 1948 linalosisitiza haki ya elimu, Sera ya Haki za Mtoto ya mwaka 1989 ihusuyo mataifa kutoa elimu kwa watoto wote na Sera ya Elimu kwa Wote ya mwaka 1990 inayolenga utoaji wa elimu bila kujali tofauti za kimaumbile. Kadhalika, Mtaala umezingatia Kanuni za Umoja wa Mataifa za fursa sawa kwa watu wenye ulemavu za mwaka 1994 zinazohimiza fursa sawa katika utoaji wa elimu ya msingi, sekondari na vyuo kwa watoto, vijana na watu wazima wenye mahitaji maalumu. Aidha, Mtaala umezingatia kuwapo kwa malengo ya Maendeleo ya Milenia ya mwaka 2000, kipengele cha 2 na 3 vinavyotoa haki ya elimu kwa watoto wote na elimu ya jinsia ambayo inalenga kuendeleza na kukuza ujifunzaji unaozingatia kuimarisha ukuzaji wa uchumi, viwanda, ugunduzi, ajira na kuwa na uwiano sawa katika uzalishaji.

Pia, malengo ya Maendeleo Endelevu ya 2015-2030, namba 4 na 5 yanasisitiza kuhakikisha kunakuwapo elimu jumuiishi ambayo ni bora kwa wote katika kukuza ushiriki wa wadau katika elimu. Vilevile, yanasisitiza kuimarisha uwazi miongoni mwa watendaji, matumizi bora ya rasilimali, uwekaji na usimamizi wa mipango, tathmini na utekelezaji wa malengo ya sekta ndogo za elimu, ikiwemo elimu ya msingi, sekondari, ualimu na ufundi. Malengo haya endelevu yanalenga katika kuwapo kwa elimu jumuiishi na yenye uwiano kwa ngazi zote za elimu na fursa za elimu endelevu. Kati ya malengo hayo 17, lengo namba nne (4) linaasisitiza kuhakikisha utoaji wa elimu bora na yenye usawa kwa wote na kutoa fursa kwa wote katika elimu endelevu ili kukuza ujifunzaji. Hata hivyo, kati ya malengo hayo 17, saba yanajikita katika uzingatiaji wa ujumuishi. Malengo hayo ni: Kuondoa umaskini na kuboresha kilimo, usalama wa chakula na lishe; kudumisha mifumo ya maisha ili kuimarisha afya na hali bora kwa watu wa rika zote; kuhakikisha elimu bora inatolewa kwa watu wote; kudumisha haki na usawa ndani ya nchi na baina ya nchi na nchi pamoja na kuboresha makazi ya watu kuwa salama, yenye amani na yaliyo katika mifumo ya haki. Hali kadhalika, yanahimizwa pia masuala ya kuhakikisha upatikanaji wa nishati salama, maji safi na salama na usafi wa mazingira kwa watu wote.

Malengo mengine ni pamoja na kuimarisha ukuzaji wa uchumi, viwanda, ugunduzi, ajira, uwiano katika uzalishaji na matumizi na ujenzi wa miundombinu; na kudhibiti mabadiliko ya hali ya hewa, ukuzaji bora wa mazingira, matumizi mazuri ya rasilimali za majini, mfumo wa teknolojia na kuhakikisha wanyama na mimea wanakaa pamoja kwa kutegemeana.

### **2.3.2 Sera za Kitaifa**

Elimu ya Kujitegemea ndiyo sera kuu ya kitaifa ambayo inasisitiza ugunduzi na ubunifu, kujiamini, stadi za utatuzi, kuunganisha nadharia na vitendo, ujasiriamali, teknolojia na udadisi katika elimu. Falsafa hii ya elimu ya kujitegemea imejitokeza katika sera mbalimbali za elimu ambazo zinatumika katika utoaji wa elimu nchini, hususani hizi zifuatazo:

#### **2.3.2.1 Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014**

Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 imesisitiza upatikanaji wa elimu na mafunzo kwa watu wote bila kujali jinsia, rangi, kabila, dini, ulemavu na hali ya kijamii au kipato. Pia kuwapo mfumo wa elimu na mafunzo unaozingatia masuala mtambuka yakiwamo elimu ya mazingira na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (VVU). Kwa mujibu wa Sera ya Elimu ya Mafunzo ya Mwaka 2014, lugha rasmi ya kufundishia Elimu ya Msingi pamoja na maandalizi ya walimu tarajali wa vyuo vya ualimu ngazi ya Astashahada ni Kiswahili, na lugha ya Kiingereza itafundishwa kama somo la lazima. Sera pia imesisitiza uandaaji wa walimu mahiri ili kukidhi mahitaji ya sekta ya elimu. Hivyo, Mtaala wa Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu umeandaliwa ili kukidhi matakwa ya kisera ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014.

#### **2.3.2.2 Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025**

Dira ya Maendeleo ya Taifa kufikia mwaka 2025 imelenga kukuza maendeleo ya jamii, hususani kutoa elimu bora kwa lengo la kuendeleza walengwa katika ubunifu, ugunduzi au uvumbuzi, maarifa na stadi mbalimbali ili kupata wataalamu wenye uwezo wa kutatua matatizo ya jamii, kukuza utumiaji wa sayansi na teknolojia na utoaji wa elimu kwa vitendo katika ngazi zote.

### **2.3.2.3 Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA)**

Mtaala huu pia umezingatia malengo yaliyomo katika Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA) ambao umelenga kuwa na mfumo wa elimu utakaowapa walengwa maarifa, stadi na mielekeo chanya ya kushiriki vyema katika kujiletea maendeleo yao wenyewe. Hali hiyo italeti tija kwa mtu binafsi na kwa taifa kwa ujumla na hivyo kupunguza umaskini.

### **2.3.2.4 Sera ya Huduma na Maendeleo kwa Watu wenye Ulemavu ya mwaka 2004**

Sera ya Huduma na Maendeleo kwa Watu wenye Ulemavu ya mwaka 2004 inalenga upatikanaji wa huduma za afya, elimu, ajira, habari na uandaaji wa mazingira rafiki kwa watu wenye ulemavu. Hivyo, sera inasisitiza watu wenye ulemavu kupatiwa mafunzo ya stadi za maisha ili waweze kujitegemea na kumudu mazingira wanayoishi.

### **2.3.2.5 Sheria ya watu wenye Ulemavu ya mwaka 2010**

Sheria ya watu wenye ulemavu namba 9 ya mwaka 2010 inasisitiza utoaji wa elimu kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu.

### **2.3.2.6 Mkakati wa Taifa wa Elimu Jumuishi wa Mwaka 2018-2021**

Mkakati wa Taifa wa Elimu Jumuishi wa mwaka 2018-2021 unalenga katika kuhakikisha kuwa watoto wote, vijana na watu wazima wanapata elimu iliyo bora na kwa usawa katika mazingira jumuishi. Mkakati huu unasisitiza ufundishaji na ujifunzaji unaozingatia mahitaji ya ujifunzaji wa watoto wote, msaada wa kielimu kwa kila mwanafunzi, kuongeza na kuboresha uwezeshwaji wa kitaalamu wa watoa elimu na kuimarisha ushiriki wa jamii katika utoaji wa elimu jumuishi.

### **3.0 Dira, Dhamira, Malengo na Ujuzi wa Jumla wa Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu**

#### **3.1 Dira**

Elimu ya Ualimu Elimu Maalumu inalenga kuwa na mwalimu mahiri, mbobezi na mwenye maarifa, stadi na mwelekeo chanya atakayeweza kuwahudumia wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika kuwezesha ujifunzaji wao.

#### **3.2 Dhamira**

Kuwa na miundombinu bora na kutoa rasilimali za kutosha ili kuandaa walimu wa Elimu Maalumu wa shule za msingi wenye sifa za kitaaluma, wawajibikaji, nyumbufu na mahiri katika kuweka mazingira bora yanayomjali mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu katika ujifunzaji wenye ujenzi wa umahiri.

### **3.3 Malengo ya Jumla ya Elimu, Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu na Ualimu Elimu Maalumu**

#### **3.3.1 Malengo ya Elimu Nchini Tanzania**

Elimu inayotolewa ni ya kurithisha maarifa, stadi na mielekeo bora kutoka kwa vizazi vilivyopita hadi vizazi vya wakati huu na vijavyo. Hivyo, yafuatayo ndiyo malengo ya elimu nchini:

- a) Kuelekeza na kukuza maendeleo, kuboresha haiba ya wananchi wa Tanzania, rasilimali zao na matumizi bora ya rasilimali hizo katika kuleta maendeleo ya mtu binafsi na ya kitaifa;
- b) Kukuza tabia ya kuthamini utamaduni, mila na desturi za watanzania;
- c) Kukuza upatikanaji wa fursa za kusoma, kuandika na kuhesabu na matumizi sahihi ya maarifa na stadi za kijamii, kisayansi, kiufundi, kiteknolojia, kitaalamu na aina nyingine za maarifa na ujuzi, kwa ajili ya maendeleo na kuboresha hali ya mtu na jamii;
- d) Kukuza na kuendeleza kujiamini, kudadisi, weledi na kuheshimu utu wa mtu na haki za binadamu na kuwa tayari kufanya kazi kwa kujiendeleza na kwa maendeleo ya Taifa;
- e) Kuwezesha na kupanua mawanda ya kujipatia maarifa, kuboresha na kukuza stadi za kiakili, utendaji, uzalishaji na nyingine zinazotakiwa katika kukidhi mabadiliko ya mahitaji kiuchumi;

- f) Kumwezesha kila raia kuelewa misingi ya katiba ya nchi pamoja na kuthamini haki za binadamu na uraia, wajibu na majukumu yanayoendana nayo;
- g) Kukuza utashi wa kupenda na kuheshimu kazi za kujiajiri na kuajiriwa na kuboresha utendaji kazi katika sekta za uzalishaji na huduma;
- h) Kujenga misingi ya maadili yanayokubalika kitaifa na ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na sheria kwa njia ya kujifunza;
- i) Kuwezesha kuwapo kwa matumizi sahihi, usimamizi na utunzaji wa mazingira; na
- j) kujenga tabia na utamaduni wa kuwakubali watu wenye ulemavu na kuwashirikisha kwenye nyanja zote za maisha kwa maendeleo ya Taifa.

### **3.3.2 Malengo ya Jumla ya Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu**

Mafunzo ya Ualimu Elimu Maalumu yana malengo yafuatayo:

- a) Kujenga umahiri kwa mwalimu tarajali katika nadharia za saikolojia ya elimu, malezi, ushauri na huduma kwa watu wenye ulemavu;
- b) Kujenga umahiri kwa mwalimu tarajali katika kugundua na kubuni njia na mbinu za kufundishia na kujifunzia;
- c) Kujenga umahiri kwa mwalimu tarajali katika uchambuzi wa mtaala na vifaa vya mtaala;
- d) Kujenga umahiri kwa mwalimu tarajali katika kumudu stadi kuu za masomo ya lugha, sanaa na maendeleo ya sayansi na teknolojia;
- e) Kujenga umahiri kwa mwalimu tarajali katika kufanya upimaji na tathmini ya maendeleo katika elimu;
- f) Kujenga umahiri kwa mwalimu tarajali katika stadi za uongozi na utawala katika elimu; na
- g) Kujenga umahiri wa mwalimu tarajali katika kumfundisha mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu.



### **3.3.3 Madhumuni ya Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu**

Mwishoni mwa mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu ya miaka miwili, mwalimu tarajali aweze:

- a) Kutafsiri mtaala wa elimu ya msingi na mihtasari yake katika masomo darasani;
- b) Kuandaa na kutumia njia shirikishi katika ujifunzaji/ufundishaji kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi;
- c) Kubuni, kuendeleza na kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia katika elimu ya msingi kwa kuzingatia mahitaji ya Mwanafunzi;
- d) Kufanya tafiti tatu za wanafunzi ili kuwabaini na kuwasaidia wale wenye mahitaji maalumu katika shule za msingi.
- e) Kurithisha desturi, maadili na tabia zinazokubalika kwa wanafunzi wa shule za msingi;
- f) Kuchagua, kupanga, kusimamia na kuongoza vipindi darasani katika shule za msingi;
- g) Kufundisha kwa ufanisi masuala mtambuka; na
- h) Kutunga na kusahihisha majaribio na mitihani inayoendana na mtaala wa elimu ya msingi kwa kuzingatia mahitaji ya Mwanafunzi katika nyanja zote tatu za kujifunza.

### **3.3.4 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu**

Umahiri mkuu wa mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu umejikita katika kumuandaa mwalimu tarajali aweze:

- a) Kumbaini mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu, kujenga misingi ya kukubalika kwake, kwa wenzake, kwa jamii na kumpatia afua stahiki;
- b) Kutumia mazingira wezeshi ya ufundishaji na ujifunzaji kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu;
- c) Kutumia njia mbalimbali za mawasiliano na teknolojia saidizi kwa kuzingatia mahitaji maalumu ya mwanafunzi;
- d) Kutumia mbinu mbalimbali katika kutambua vipaji walivyonavyo wanafunzi wenye mahitaji maalumu na namna ya kuyiendeleza;

- e) Kufanya tafiti tatuzi za kielimu kwa wanafunzi ili kuwabaini na kuwasaidia wale wenye mahitaji maalumu katika shule za msingi;
- f) Kutumia misingi na stadi za uongozi katika kuongoza taasisi mbalimbali za elimu;
- g) Kutumia, kutunza na kukarabati vifaa saidizi vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu;
- h) Kutumia sanaa na michezo rekebifu katika kuibua vipaji mbalimbali vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu;
- i) Kutumia misingi ya ufundishaji na ujifunzaji kufundishia masomo ya taaluma;
- j) Kujenga umahiri wa masomo kwa mwalimu tarajali utakaomuwezesha kuelewa masomo vema na hivyo kumfundisha mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu; na
- k) Kushirikiana na familia za wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika kuwajengea wanafunzi hao kujiamini, tabia ya kujifunza na kukuza vipaji walivyonavyo.

## **4.0 Muda wa Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu**

### **4.1 Miaka ya Mafunzo**

Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu yatakuwa ni ya miaka miwili kwa wanafunzi waliomaliza Elimu ya Sekondari Kidato cha Nne na kufaulu katika daraja la I hadi la III. Mwishoni mwa ngazi hii, walimu tarajali wanaweza kuendelea na mafunzo ya stashahada au kuingia kwenye ulimwengu wa kazi.

### **4.2 Muda wa Masomo**

Katika mafunzo haya, muda wa masomo utakuwa kama ifuatavyo:

- a) Kila kipindi kitakuwa ni cha saa moja.
- b) Kutakuwa na vipindi saba kwa siku.
- c) Sehemu ya siku inayobaki itatumika kwa shughuli za nje.

### **4.3 Mihula ya Masomo**

- a) Mwaka wa masomo utakuwa na siku 194.
- b) Kutakuwa na mihula miwili kwa mwaka ambayo itakuwa na majuma 19 kila mihula.
- c) Mafunzo ya Ualimu Elimu Maalumu yatakuwa ni ya miaka miwili na kuwa na jumla ya mihula minne.
- d) Kutakuwa na Mafunzo ya Ualimu kwa Vitendo ya siku 60 kwa mwaka wa kwanza na wa pili.

**Tanbihi:** Mwalimu tarajali atakayekuwa nje ya masomo kwa muda wa siku 65 mfululizo kwa mwaka hataruhusiwa kuendelea na masomo.

### **5.0 Muundo wa Maudhui, Maeneo na Masomo ya Kujifunza**

Mtaala wa Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu umeandaliwa kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri ambapo msingi wa ufundishaji unajengwa katika vitendo vinavyojenga umahiri badala ya nadharia. Muundo wa maudhui, maeneo na masomo ya kujifunza utatofautiana kutoka fani moja hadi nyingine. Maeneo ya kujifunza kwa mwalimu tarajali wa Elimu Maalumu yatakuwa kama ifuatavyo:

- a) Masomo ya Elimu Maalumu (Masomo ya Fani)
- b) Somo la Ualimu (Somo la lazima)
- c) Masomo ya Ufundishaji (Kuchagua)
- d) Somo la Elimu Jumuishi (Somo la lazima)

Mwalimu tarajali atapaswa kusoma masomo ya fani aliyochagua, masomo ya mchepuo aliouchagua kati ya Lugha, Sayansi, Hisabati na Maarifa ya Jamii. Somo la Ualimu na somo la Elimu Jumuishi yatakuwa ni ya lazima; kwa hiyo, idadi ya masomo atakayosoma mwalimu tarajali itakuwa ni masomo kati ya tisa hadi kumi na tatu kutegemeana na fani aliyochagua.

Jedwali 1: Mchanganuo wa Vipindi kwa Wiki kwa Fani na Mchepuo

Fani	Mchepuo	Vipindi vya Masomo ya Mchepuo	Vipindi vya Masomo ya Kufundishia	Jumla ya Vipindi kwa Wiki
Ulemavu wa uoni	Lugha	15	17	32
	Sayansi	15	17	32
	Sayansi ya Jamii	15	16	31
Uziwi	Lugha	16	17	33
	Sayansi	16	16	32
	Sayansi ya Jamii	16	15	31
Ulemavu wa Akili na usonji	Lugha	16	17	33
	Sayansi	16	16	32
	Sayansi ya Jamii	16	15	31

### 5.1 Masomo ya Fani za Ualimu Elimu Maalumu

Mwalimu tarajali atapaswa kusoma masomo ya fani mojawapo aliyoichagua kutoka katika fani kama zilivyooneshwa kwenye Jedwali la 1.

Jedwali la 2: Masomo katika Fani ya Ualimu Elimu Maalumu

Na.	Fani	Masomo	Idadi ya Vipindi (saa) kwa Wiki
1	Ulemavu wa uoni	1.1 Stadi za Mawasiliano kwa Wanafunzi wenye Ulemavu wa Uoni	4
		1.2 Mafunzo Kabilishi na Mjongeo	2
		1.3 Michezo na Sanaa Rekebifu	2
		1.4 Anatomia, Fiziolojia na Patholojia ya Jicho	2
		1.5 Utunzaji na Ukarabati wa Vifaa vya Kielimu	3
		1.6 Ujifunzaji wa Mwanafunzi Mwenye Uziwikutoona	2
		<b>Jumla ya Vipindi kwa Wiki</b>	

<b>Na.</b>	<b>Fani</b>	<b>Masomo</b>	<b>Idadi ya Vipindi (saa) kwa Wiki</b>
2	Uziwi	2.1 Stadi za Mawasiliano	2
		2.2 Audiolojia	4
		2.3 Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT)	4
		2.4 Michezo na Sanaa Rekebifu	2
		2.5 Utunzaji na Ukarabati wa Vifaa vya Audiolojia	2
		2.6 Ujifunzaji wa Mwanafunzi Mwenye Uziwikutoona	2
		<b><i>Jumla ya Vipindi kwa Wiki</i></b>	<b>16</b>
3	Ulemavu wa Akili na usonji	3.1 Ufundishaji na Ujifunzaji wa Mwanafunzi mwenye Ulemavu wa Akili	3
		3.2 Stadi za Mawasiliano kwa Mwanafunzi mwenye Ulemavu wa Akili	3
		3.3 Upimaji na Afua Stahiki kwa Mwanafunzi mwenye Ulemavu wa Akili	3
		3.4 Michezo na Sanaa Rekebifu	3
		3.5 Ufundishaji na Ujifunzaji wa Mwanafunzi mwenye usonji	4
		<b><i>Jumla ya Vipindi kwa Wiki</i></b>	<b>16</b>

## 5.2 Masomo ya Ufundishaji

Mwalimu tarajali atapaswa kujifunza ufundishaji wa masomo ya shule ya msingi kwa kuchagua mchepuo mmoja kutoka michepuo ifuatayo:

Jedwali la 3: Michepuo na Masomo ya Ufundishaji katika Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu

Na.	Mchepuo	Somo	Idadi ya Vipindi (saa) kwa Wiki
1	Lugha	Kiswahili	2
		Kiingereza	2
		Stadi za Kazi	2
		Ualimu	3
		Elimu Jumuishi	2
		Uraia na Maadili	1
		Stadi za Mawasiliano	2
		TEHAMA	2
		Dini	1
		<b><i>Jumla ya Vipindi kwa Wiki</i></b>	<b>17</b>
2	Sayansi	Hisabati	2
		Sayansi na Teknolojia	2
		Stadi za Kazi	2
		Uraia na Maadili	1
		Stadi za Mawasiliano	2
		TEHAMA	2
		Ualimu	3
		Dini	1
		Elimu Jumuishi	2
		<b><i>Jumla ya Vipindi kwa Wiki</i></b>	<b>17</b>
3	Sayansi ya Jamii	Maarifa ya Jamii	3
		Uraia na Maadili	1
		Stadi za Kazi	2
		Stadi za Mawasiliano	2
		TEHAMA	2
		Ualimu	3
		Dini	1
		Elimu Jumuishi	2
<b><i>Jumla ya Vipindi kwa Wiki</i></b>	<b>16</b>		

Jedwali la 4: Umahiri Mkuu wa Masomo ya Fani kwa Mwalimu Tarajali

FANI	SOMO	UMAHIRI MKUU
Ulemavu wa Uoni	Stadi za Mawasiliano	Kutumia stadi za mawasiliano kulingana na mahitaji ya mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni Kutumia mbinu mbalimbali kuwezesha ufundishaji wa stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kumwezesha mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni kuwasiliana Kutumia stadi za Breli kumwezesha mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni kuwasiliana
	Mafunzo Kabilishi na Mjongoe	Kutumia stadi za mafunzo kabilishi kumwezesha mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni kuyamudu mazingira Kujenga stadi za ujongaji ili kumwezesha mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni kuyamudu mazingira Kutumia stadi za mafunzo kabilishi na ujongaji ili kujenga stadi za maisha kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni
	Michezo na Sanaa Rekebifu	Kutumia stadi za michezo rekebifu kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni Kutumia elimu ya viungo katika kuimarisha viungo kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni. Kutumia sanaa mbalimbali kukuza na kuibua vipaji kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni.
	Anatomia, Fiziolojia na Patholojia ya Jicho	Kutumia sayansi ya jicho kubaini mahitaji ya mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni Kutumia sayansi ya jicho kubaini visababishi vya ulemavu wa uoni Kutumia sayansi ya jicho kuchambua hitilafu katika jicho Kutumia mbinu za upimaji katika kutoa afua stahiki kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni
	Utunzaji na Ukarabati wa Vifaa vya Kielimu	Kutengeneza vifaa vya kielimu vya wanafunzi wenye ulemavu wa uoni Kukarabati vifaa vya kielimu Kutunza vifaa vya wanafunzi wenye ulemavu wa uoni Kukarabati mashine za Breli

FANI	SOMO	UMAHIRI MKUU
	Ujifunzaji wa Mwanafunzi mwenye uziwikutoona	Kufafanua dhana ya uziwikutoona
		Kutumia stadi za mawasiliano kulingana na mahitaji ya mwanafunzi mwenye uziwikutoona
		Kutumia njia za ufundishaji na ujifunzaji kulingana na mahitaji ya mwanafunzi mwenye uziwikutoona
		Kukuza stadi za elimu ya michezo na sanaa rekebifu kwa mwanafunzi mwenye uziwikutoona
		Kuimarisha mafunzo kabilishi na ujongeaji wa mwanafunzi mwenye uziwikutoona
Uziwi	Stadi za Mawasiliano	Kutumia stadi za mawasiliano kulingana na mahitaji ya mwanafunzi kiziwi
		Kutumia stadi za ukalimani wa Lugha ya Alama kumuwezesha mwanafunzi kiziwi kuwasiliana
		Kutumia stadi za mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi
		Kutumia mbinu mbalimbali kuwezesha ufundishaji wa stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa kumuwezesha mwanafunzi kiziwi kuwasiliana
		Kutumia sayansi ya usikivu kubaini mahitaji ya mwanafunzi kiziwi
	Audiolojia	Kutumia sayansi ya usikivu, kubaini visababishi vya uziwi
		Kutumia sayansi ya usikivu, kuchambua kasoro za sikio
		Kutumia mbinu za upimaji kutoa afua stahiki kwa mwanafunzi kiziwi
	Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT)	Kutumia mazingira ya lugha kueleza hali, historia na maendeleo ya Lugha ya Alama ya Tanzania
		Kutumia kanuni za LAT kuunda alama za msingi
		Kutumia kanuni za LAT kuwasiliana kwa ufasaha
		Kutumia stadi za lugha kukuza mawasiliano ya LAT katika taaluma
	Michezo na Sanaa Rekebifu.	Kutumia stadi za michezo na sanaa rekebifu kwa mwanafunzi kiziwi



FANI	SOMO	UMAHIRI MKUU
		Kutumia elimu ya mazoezi ya viungo katika kuimarisha viungo kwa mwanafunzi kiziwi
		Kutumia sanaa mbalimbali kukuza na kuibua vipaji kwa mwanafunzi kiziwi
	Ujifunzaji wa Mwanafunzi mwenye uziwikutoona	Kufafanua dhana ya uziwikutoona
		Kutumia stadi za mawasiliano kulingana na mahitaji ya mwanafunzi mwenye uziwikutoona
		Kutumia njia za ufundishaji na ujifunzaji kulingana na mahitaji ya mwanafunzi mwenye uziwikutoona
		Kukuza stadi za elimu ya michezo na sanaa rekebifu kwa mwanafunzi mwenye uziwikutoona
		Kuimarisha mafunzo kabilishi na ujongaji wa mwanafunzi mwenye uziwikutoona
	Utunzaji na Ukarabati wa Vifaa vya Audiolojia	Kutengeneza vifaa vya audiolojia
		Kukarabati vifaa vya audiolojia
		Kutunza vifaa vya Audiolojia
Ulemavu wa Akili na Usonji	Ufundishaji na Ujifunzaji wa Mwanafunzi mwenye Ulemavu wa Akili	Kutumia stadi za anatomia na fiziolojia kuchambua utendaji kazi wa mfumo wa neva
		Kutumia maarifa na ujuzi kumpatia mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili mahitaji yake katika ujifunzaji
		Kumpatia mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili mahitaji yake katika ujifunzaji
		Kutumia mbinu mbalimbali za kumfundishia mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili
	Stadi za Mawasiliano	Kutumia njia za mawasiliano na teknolojia saidizi kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji
		Kuchambua ala za matamshi
		Kufanya upimaji na kutoa afua stahiki za mawasiliano kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji
		Kutumia stadi rekebifu katika mawasiliano kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji

FANI	SOMO	UMAHIRI MKUU
		<p>Kuchunguza dosari/hitilafu katika lugha kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji</p> <p>Kutumia msingi wa elimu ya Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) katika kuwezesha kusoma, kuandika na kuhesabu</p>
	Upimaji na Afua Stahiki	<p>Kufanya upimaji kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji</p> <p>Kutumia vifaa na zana za upimaji kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji</p> <p>Kutumia stadi za upimaji kutoa afua stahiki kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji</p> <p>Kuandaa hatua za mpito kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji</p>
	Michezo na Sanaa Rekebifu	<p>Kutumia elimu ya michezo rekebifu kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji</p> <p>Kutumia elimu ya sanaa rekebifu kwa wanafunzi wenye ulemavu wa akili na wanafunzi wenye usonji</p> <p>Kutumia elimu ya viungo rekebifu katika kurekebisha viungo kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji</p> <p>Kutumia milango ya fahamu kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji</p>
	Ufundishaji na Ujifunzaji wa Mwanafunzi mwenye Usonji.	<p>Kutumia stadi za anatomia na fiziolojia kuchambua utendaji kazi wa mfumo wa neva</p> <p>Kumbaini mwanafunzi mwenye usonji</p> <p>Kutumia maarifa na ujuzi kumpatia mwanafunzi mwenye usonji mahitaji yake katika ujifunzaji</p> <p>Kutumia mbinu mbalimbali za kumfundishia mwanafunzi mwenye usonji</p>

Jedwali la 5: Umahiri wa Jumla wa Somo na Umahiri Mkuu wa kila Fani kwa Masomo ya Ufundishaji kwa Mwalimu Tarajali

<b>Na</b>	<b>SOMO</b>	<b>UMAHIRI WA JUMLA</b>	<b>FANI</b>	<b>UMAHIRI MKUU</b>
1	Kiswahili	Kutumia nadharia mbalimbali za Kiswahili katika kujifunza na kufundisha.	Ulemavu wa Uoni na Uziwikutoona	Kutumia vifaa vya mtaala kwa kuzingatia mahitaji maalumu ya mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni na Mwanafunzi mwenye uziwikutoona.
		Kutumia zana za upimaji katika ujifunzaji.		Kutumia njia na mbinu za ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni na Mwanafunzi mwenye uziwikutoona.
		Kukuza stadi za lugha katika mawasiliano.		Kutumia zana za ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji maalumu ya mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni na mwanafunzi mwenye uziwikutoona.
			Uziwi na Uziwikutoona	Kutumia vifaa vya mtaala kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi mwenye uziwi na mwanafunzi mwenye uziwikutoona.
				Kuchambua mbinu na njia za kufundishia na kujifunzia mwanafunzi mwenye uziwi na mwanafunzi mwenye uziwikutoona.

Na	SOMO	UMAHIRI WA JUMLA	FANI	UMAHIRI MKUU
				Kutumia zana za Ufundishaji na Ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi mwenye uziwi na mwanafunzi mwenye uziwikutoona.
				Kushirikisha wadau katika kutambua changamoto na kutoa huduma kwa mwanafunzi mwenye uziwi na mwanafunzi mwenye uziwikutoona.
			Ulemavu wa Akili na Usonji	Kutumia njia na mbinu za kufundishia na kujifunzia mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji.
				Kutumia vifaa vya mtaala kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji.
				Kueleza umuhimu wa matumizi ya zana za ufundishaji na ujifunzaji kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji.

Na	SOMO	UMAHIRI WA JUMLA	FANI	UMAHIRI MKUU
				Kutumia njia na mbinu za kumudu darasa (hatua) kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji.
				Kuandaa mipango ya ufundishaji na ujifunzaji kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji.
2	English	Analyse theoretical approaches to English language learning for learners with special needs	Visual Impaired and deafblindness	Using curriculum materials based on the needs of visually impaired and deafblind learners
		Analyse curriculum materials for teaching and learning of learners with special needs		Using teaching methods and techniques according to the needs of the visually impaired and deafblind learners
		Develop skills in comprehending information among learners with special needs		Using teaching aids according to the needs of visually impaired and deafblind learners
		Apply evaluation skills in teaching English language for learners with special needs	Hearing Impaired and Deaf-blind Learners	Using curriculum materials based on the needs of hearing impaired and deafblind learners

Na	SOMO	UMAHIRI WA JUMLA	FANI	UMAHIRI MKUU
				Using teaching methods and techniques according to the needs of the hearing impaired and deafblind learners
				Using teaching aids according to the needs of a hearing impaired and deafblind learners
			Intellectual Impairment and Autism Learners	Using curriculum materials based on the needs of learners with intellectual Impairment and autism
				Using teaching methods and techniques according to the needs of learners with intellectual Impairment and autism
				Using teaching aids according to the needs of learners with intellectual Impairment and autism
3	Hisabati	Kuchambua misingi ya ufundishaji wa somo la Hisabati kulingana na mahitaji maalumu ya mwanafunzi.	Ulemavu wa Uoni na Uziwikutoona	Kuchambua sera na vifaa vya mtaala katika somo la Hisabati kulingana na mahitaji ya mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni na mwanafunzi mwenye uziwikutoona.
		Kutumia hisabati kutatua matatizo katika mazingira tofauti kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu.		

Na	SOMO	UMAHIRI WA JUMLA	FANI	UMAHIRI MKUU	
		Kupima ujifunzaji wa somo la Hisabati na umuhimu wake.		Kutumia njia na mbinu za ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni na mwanafunzi mwenye uziwikutoona.	
				Kutumia zana za ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni na mwanafunzi mwenye uziwikutoona.	
				Uziwi na Uziwikutoona	Kuchambua vifaa vya mtaala katika somo la Hisabati kulingana na mahitaji ya mwanafunzi mwenye uziwi na mwanafunzi mwenye uziwikutoona.
					Kutumia njia na mbinu za kufundishia na kujifunzia mwanafunzi mwenye uziwi na mwanafunzi mwenye uziwikutoona.
